



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UPOTOSHAJI UNAOFANYWA NA  
MTANDAO WA TANZANIA ABROAD TV**

Dodoma, 05 Septemba, 2022

Kwa muda mrefu Televisheni ya mtandaoni ijulikanayo kama Tanzania Abroad TV, kupitia ukurasa wake wa Twitter, imekuwa ikichapisha maudhui yenyе upotoshaji kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Mtandao huo umekuwa ukifanya nukuu za Mkurugenzi wa Uchaguzi ambazo si sahihi kwa kuwa maneno hayo hayajawahi kutamkwa mahali popote.

Maudhui ya mtandao huo si kwamba yanapotosha umma tu, bali yanaharibu taswira nzuri ya Tume na kusababisha tataruki mionganini mwa wananchi.

Tume inauonya mtandao huo na kuutaka kusitisha mara moja vitendo hivyo vya kiuhalifu. Tume tayari imewasilisha rasmi malalamiko yake kwa Mamlaka husika kwa ajili ya hatua zaidi.

Imetolewa na:

**IDARA YA HABARI NA ELIMU YA MPIGA KURA**